

TANZANIA / JUDGMENT

MAREJEO NO 5071 OF 2024 WEMA MTENGWA VRS TANZANIA RAILWAY CORPORATION

COURT
TANZLIIDECIDED
1 January 2024

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DIVISHENI YA KAZI DAR ES SALAAM MAREJEO NA. 5071 YA MWAKA 2024 KESI KUMBUKUMBU (REFERENCE) NA. 202403111000005071 WEMA MTENGWA A..... MLETA MAOMBI DHIDI YA TANZANIA RAILWAY CORPORATION.....MJIBU MAOMBI WA KWANZA MWANASHERIA MKUU WA SERI K A LI..... MJIBU MAOMBI WA PILI HUKUMII Tarehe ya amri ya mwisho: 07/ 05/2024 Tarehe ya hukumu: 31/ 05/2024 MLYAMBINA.J. Baada ya kutoridhishwa na Maamuzi ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (itajulikana kama Tume), Mleta Maombi amewasilisha maombi haya mbele ya Mahakama akijikita katika hoja zifuatazo:

- i. Kwamba, Muamuzi alishindwa kabisa kuoanisha ushahidi uliotolewa na pande zote mbili hivyo kufikia uamuzi usio sahihi na wa haki. ii. Kwamba, Muamuzi alishindwa kabisa kuona kuwa vielelezo vilivyotolewa na Mlalamikiwa vilikuwa havihusiani na kipindi cha madai na pia kushindwa kuona kuwa uhamisho wa Mleta Maombi na hatimaye kuachishwa kazi isivyo halali ni msingi wa "Deed of Settlement". Kwamba, Muamuzi katoa uamuzi kutokana na hoja ambayo haikuwa sehemu ya madai ya Mleta Maombi baada ya kutolewa kwa "Certificate of settlement/Non-Settlement" kutoka kwa Msuluhishi yaani fomu CMA F6. Kwamba madai yake yalikuwa "Retirement benefits and letter of retirement" yeye akaongeza hoja na kuitolea uamuzi unaopingwa sasa. Kwamba hoja hiyo ni: "endapo Mlalamikaji a/ iajiriwa upya na shirika la TRL 2007 au aliamishwa kutoka TRC". Mleta Maombi alieleza kuwa hoja tajwa hapo juu ilikuwa imeshatolewa uamuzi na Tume awamu ya kwanza pamoja na Mahakama na haikukatiwa rufaa na Mujibu Maombi. Aliongeza kuwa, kuipenyeza hoja hiyo kinyemela katika Mahakama ya chini ni kosa la kutokuheshimu maamuzi ya Mahakama za juu, hivyo Muamuzi kujipachika mamlaka ya Marejeo ambayo si yake. Kwamba, Muamuzi alijielekeza vibaya kwa kushindwa kuona kwamba 'Deed of Settlement' haikurudishwa Tume kukaziwa hukumu kama anavyodai bali kama kielelezo cha kuwa Mleta Maombi hakupewa haki yake ya Barua ya kustaafu ili barua hiyo iainishe stahiki zake kwa kipindi cha 2007 hadi 2013 anachodai kutoka kwa Mwajiri wake wa zamani TRL ambaye aiirithiwa na TRC ya sasa ya awamu ya pili.

- v. Kwamba, Muamuzi ameshindwa kuona kwamba ushahidi na vielelezo vilivyopelekwa mbele yake na mjibu mombi vinaonesha kuwa TRC awamu ya pill inajificha nyuma ya TRC awamu ya kwanza kwa kuleta kumbukumbu za kale ambapo haya ni mashirika mawili kisheria yanayojitegemea yalioanzishwa na sheria tofauti. Hivyo, TRC awamu ya pili ilitegemewa kuleta vielelezo vya TRL kuthibitisha kuwa amelipwa au la ambapo ndiyo madai ya mleta maombi kipincli cha 2007 hadi 2013. Kutokana na hoja ainishwa hapo juu Mleta Maombi anaiomba Mahakama amri zifuatazo:
- i. Kwamba, Mahakama hii iweze kurejea na kutengua uamuzi wa Tume wa tarehe 25/08/2023 katika Shauri nambari CMA/DSM/ILA/880/19 ill Mleta Maombi aweze kusikilizwa na kuagiza Mwajiri wake ampatie barua ya kustaafu kama alivyoahidi katika Deed aliyotengeneza mwenyewe na ainishe stahiki za Mleta Maombi kwa mjibu wa kanuni za Kampuni zilivyokuwa kama mstaafu kwa sababu Muamuzi alishindwa kutoa uamuzi wa haki. ii. Kwamba, Mahakama hii tukufu ione kwamba haki ya Mleta Maombi ya utumishi wake kutoka 2007 hadi 2013 ipo na walishakubaliana na Mwajiri wake wa zamani TRL ambaye alirithiwa na TRC awamu ya pili na kuandika makubaliano (Deed of Settlement) halali ambayo yalitekelezwa isipokuwa kipengele X ambacho bado. iii. Kwamba, Mahakama ione ikiwa kuna haki na stahiki nyingine anazostahili kupewa baada ya kunyimwa barua ya kustaafu katika utumishi wake TRL. Kama kuendelea kupokea mishahara tangu tarehe 01/07/2013 hadi 2015 waliandikiana Deed of Settlement kwa sababu Mwajiri alikataa kumrudisha kazini lakini anapinga utekelezaji wa Deed of Settlement. Mleta Maombi alisistiza kuwa anachodai ni kupewa barua ya kustaafu na kuainisha mafao yake. Shauri hili liliendeshwa kwa njia ya mdomo. Katika kuendesha shauri hili, Mleta Maombi aliwakilishwa na Ndugu Sammy Katerega, Mwakilishi Binafsi, ilihali Mdugu Stephen Kimaro, Wakili wa Serikali na ndugu Hamimu Nkoleye, Wakili wa Serikali Mkuu waliwakilisha Wajibu Maombi. Bwana Katerega alifanya mawasilisho ya jumla kwa hoja zote zilizoletwa mbele ya Mahakama hii. Alieleza kuwa, malipo ambayo yanadaiwa ni chanzo cha "Deed of Settlement" iliyotengenezwa na Mwajiri ambayo haijakamilika utekelezwaji wake. Kwamba, Muamuzi baada ya kupokea FOMU Na. 6 aliongeza hoja ambayo siyo mahali pake ya kujielekeza juu ya kama Wema alijariwa au hakuajiriwa. Upande wa Wajibu Maombi walipinga vikali maombi haya na kueleza kuwa maamuzi ambayo yanaombewa kurejewa tayari yametekelezeka, yameshalipwa na Mwombaji amekiri kwenye kiapo chake kuhusiana na utekelezaji wa Maamuzi hayo. Aliongeza kuwa baadhi ya malipo hayo yamethibitishwa kupitia kielelezo D1, D2, D3 and D5. Kuhusiana na uhalali wa usahihi wa uamuzi wa CMA, ilielezwa kuwa malalamiko ni kutopewa barua ya kustaafu na mafao ya kustaafu. Ilielezwa kuwa Upande wa Mdaiwa walieleza wakati huo Mleta Maombi alikuwa si mtumishi wa TRL kwani alikuwa amepunguzwa. Hii ilipelekea Mwamuzi kujielekeza kwenye hoja, je kule TRL alikuwa kwenye ajira mpya au amehamishwa? Ikatokea hoja ya kuwepo kwa barua mbili. Moja ya kumpunguza kazi na nyingine ya kumhamisha. Alieleza kuwa, Mleta maombi alianza kwa kupokea barua ya uhamisho. Baadae akapata ya kupunguzwa kazi ambayo ilikuwa inaambatana na malipo. Yeye akapokea barua iliyoambatana na malipo na malipo akapokea na akadai anaendelea na kazi. Hiyo ni mojawapo ya hoja muhimu kwa Mwamuzi

ambayo aliitolea maamuzi. Mahakama imezingatia kwa kina mawasilisho ya pande zote mbili. Katika fomu ya kuanzishia lalamiko Tume (CMA FI), Mleta Maombi ameeleza wazi kuwa anadai malipo yake ya kustaafu pamoja na barua ya kustaafu. Pia, katika maelezo yake ya awali mbele ya Tume, Mleta Maombi alifafanua kuwa anadai utekelezaji wa kifungu Namba X cha (Deed of settlement) cha masharti ya makubaliano ya tarehe 23/03/2015. Lakini hata mbele ya Mahakama hii Mleta Maombi amesisitiza hayo ndiyo madai yake aliyowasilisha mbele ya Tume na ndio kiini cha mgogoro wake uliotakiwa kutatuliwa na Tume. Baada ya kupitia aina ya madai yake, Mahakama inaunga mkono maamuzi bishaniwa. Tume haikuwa na mamlaka ya kutekeleza Makubaliano hayo kwani yalifanywa mbele ya Mahakama Kuu. Huu ndio msimamo uliowekwa na sheria. Utekelezwaji wa Makubaliano husika au maamuzi mengine yoyote ya Mahakama Kuu utafanywa na Mahakama yenyewe kama ambavyo imeelekezwa katika Kifungu cha 48 (3) cha Kanuni za Mahakama ya Kazi, Tangazo la Serikali Na. 106 la mwaka 2007. Naongeza kuwa, hata kama makubaliano hayo yangeanywa mbele ya Tume, Chombo hicho kisingekuwa na mamlaka ya kutekeleza makubaliano hayo kwani jukumu hilo ni la Mahakama kama ambavyo imeelekezwa katika Kifungu cha 89 (2) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, [Sura Namba 366 Kama Hivyorejewa mwaka 2019]. Pia, Mahakama imezingatia malalamiko ya Mleta Maombi kuwa, Mwamuzi alifanya makosa kutatua hoja ya endapo Mlalamikaji alilajiriwa upya na shirika la TRL 2007 au alihamishwa kutoka TRC. Mahakama inakubaliana na Mleta Maombi kuwa Tume ilikua haina sababu ya kujadili tena hoja hiyo kwani tayari ilishaamuriwa na pande zote mbili zikafikia makubaliano. Mleta Maombi anaomba utekelezaji wa sehemu ya makubaliano hayo. Hivyo basi, Mahakama inaona ya kuwa maombi haya hayana mantiki. Ni wazi kuwa Tume haikuwa na mamlaka ya kusikiliza mgogoro huu, hivyo ilikua sahihi kuutupilia mbali. Pia, Mahakama hii inatupilia mbali maombi haya kwakuwa hayana mantiki. Imeamuriwa hivyo. Y. J. MLYAM JAJI 31/05/2024 Hukumu hii imesomwa na kutolewa leo tarehe 31/05/2024 mbele ya Mleta Maombi, Sammy Kateregga Mwakilishi Binafsi wa Mleta Maombi na Msomi Wakili wa Serikali Mathew Fuko kwa ajili ya Wajibu Maombi\

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE	https://media.tanzlii.org/media/judgment/312469/source_file/MAREJEO_NO_5071_OF_2024_WEMA_MTENGWA_VRS_TANZANIA_RAILWAY_CORPORATION.pdf
CASE PAGE	https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/wema-mtengwa-RetirementBenefits-tanzlii-2024--6a3ea52d3b1caa91298269b7

Prepared on 13 October 2026 · Esheria